Wanafunzi wa Mount Pleasant High School Band na Kwaya wanafanya maonyesho pamoja na **Rhode Island Wind Ensemble**!

MIUNGANISHO

TAREHE 20 JANUARI, 2023

KONA YA AFISA MKUU MSIMAMIZI



DKT. JAVIER MONTAÑEZ
MSIMAMIZI

Karibu kwenye toleo jipya la Shule ya Umma ya Wilaya ya Providence (PPSD) kijarida cha mara mbili kwa wiki! Ikiwa wewe au mtu unayemjua atakosa mojawapo ya vijarida vyetu, unaweza kupata matoleo ya awali kwenye tovuti ya Wilaya katika lugha nyingi.

Ningependa kuanza toleo hili la kijarida kwa asante kutoka moyoni kwa wana bodi watatu wa Shule ambao miadi yao inaisha mwezi huu. Raisi wa Bodi Kinzel Thomas, Raisi Msaidizi Diagneris Garcia, na mwana bodi Jesús Núñez wamekuwa wakili wakali kwa jamii ya PPSD.

Jambo zuri ni kwamba hii sio kwa heri, kwa sababu kila mmoja wa mwana bodi hii ataendelea kuonekana na kuwa adilifu Wilayani. Tunajua watachukulia washika dau wote kuwajibika kwa kutengeneza PPSD ambayo wanafunzi wetu, familia na walimu wanastahiki.

Pia tuna ngoja kwa hamu kwa kukaribisha washiriki wapya wa Bodi ya Shule na maoni na uzoefu mwezi ujao. Mabadiliko ni sehemu ya kukua na kufanya maendeleo, na nangoja kwa hamu kufanya kazi pamoja kufanya Mpango wetu wa Kubadilisha Jumuiya kuwa ukweli. Muungano huu ni muhimu hususan wakati tunapo badilisha Wilaya kwa muda mzuri wa uwekezaji shuleni mwetu.

Kama vile Gavana McKee alivyo ashiria katika hotuba yake kwa Jimbo mwezi huu, PPSD imepanga kutoka kwa 5% ya wanafunzi katika majengo bora hadi kwa 50% katika miaka ijayo. Mabadiliko kama haya ni nadra kuwa rahisi, lakini ni muhimu sana kwa wanafunzi wetu.

TAARIFA MPYA ZA WILAYA

SIKU YA KUONDOKA MAPEMA TAREHE 25 JANUARI

Huu ni ukumbusho wa kirafiki kwamba **shule zote** zitakuwa na muda mwingine wa kuruhusiwa kuondoka mapema wa saa mbili kila mwezi siku ya **Jumatano, tarehe 25 Januari**, kwa ajili ya maendeleo ya kitaalamu ya walimu. Familia za shule za kati zinapaswa kutambua kwamba hii ni tofauti na wakati wa kawaida wa kuruhusiwa kuondoka Jumatano kwa wanafunzi wa shule ya kati. Hii inaruhusu mabasi kukimbia kwa wakati kwa shule zingine ambazo pia huondolewa mapema siku hiyo. Familia zinapaswa pia kukumbuka kuangalia mara mbili ratiba katika vituo vya burudani vya ndani, kwani vingine vinaweza kufungwa hadi saa tisa alasiri (3 p.m.) kwa sababu ya wafanyakazi.

MAONYESHO YA KANDARASI YA KUAJIRI MAPEMA

PPSD kwa sasa inapeana kandarasi ya kuajiri mapema katika sehemu zenye changamoto zaidi kujaza kwa mwaka wa shule 2023/2024. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu mpango hapa tinyurl.com/ppsdearly23. Wagombeaji waliochaguliwa wanastahiki kwa vichocheo vya ajira na pakiti za bonasi kwa kujaza sehemu zenye changamoto za kujaza. Wagombeaji pia watakuwa na fursa ya kusikiza kutoka kwa meneja wa kuajiri kutoka kwa mtandao wa PPSD. Wagombeaji wanaweza kusajili katika tinyurl.com/PPSDearlyhiring.

KUMBUSHO MUHIMU KUJAZA UTAFITI WA MAPATO YA KAYA

Wanafunzi wote wa PPSD wamestahiki kupokea kiamsha kinywa na chakula cha mchana bila malipo. Lakini, kila mwaka familia Wilayani ni lazima wajaze Utafiti wa faragha wa Mapato ya Kaya kuhakikisha manufaa haya. Familia ambao hawaja jaza Utafiti wa Mapato ya Kaya watapokea kumbusho kutoka Wilaya kufanya hivyo kupitia ujumbe mfupi kupitia Kinvo na mawasiliano kutoka shuleni mwao. Taarifa ya familia ni ya faragha na haita shirikishwa. Ikiwa huja fanya hivyo, tafadhali kamilisha utafiti na urejeshe katika shule ya mtoto wako ili wanafunzi waendelee kupokea kiamsha kimya bila malipo. Asante!

MPANGO WA UPANUZI WA LUGHA MBILI

Shule za Umma za Providence zina panua uchaguzi wa mpango wa Lugha Mbili Wilayani kote katika madarasa ya kabla ya shule ya chekechea hadi 12. Katika bidii ya kujenga ufahamu wa modeli za mpango na kupeana nafasi kwa bidii, Afisi ya Wanafunzi wa Lugha Nyingi ingependa kukukaribisha kibinafsi, mshirika wa thamani wa jumuiya ya Shule za Umma za Providence, kushiriki katika utafiti unao kuja. Data kutoka kwa utafiti utasaidia mchakato wa kufanya maamuzi kwa mipango ya Lugha Mbili katika PPSD siku zijazo. **Bofya hapa kufikia utafiti: https://rezed.io/1NLV0T**

USAWA KWA FURSA KATIKA SHULE ZA UMMA ZA PROVIDENCE

Tazama habari za hivi majuzi kabisa katika Tovuti kwenye Kijarida cha Usawa hapa >

KUANGAZWA KWENYE FAMILIA MOJA YETU YA PPSD

Brian Johnson ana umri wa miaka 31 na ni mchezaji wa Olimpiki Maalum wa Rhode Island. Brian amechaguliwa kuhudhuria **Michezo ya Dunia ya Olimpiki Maalum** huko Berlin, Ujerumani kwa siku 17 mnamo Juni 2023. Brian ata cheza bocce akiwa pamoja na mshiriki mwenzake aliye unganishwa naye. Brian alikuwa mchezaji wa kipekee kutoka Rhode Island aliyechaguliwa kushiriki katika michezo hiyo. Watakao hudhuria michezo itakuwa wachezaji 7,500 na washiriki walio unganishwa, wanao wakilisha nchi 170! Olimpiki Maalum ya Marekani ita tuma timu ya kadiria 225 kutoka Marekani kote. Hii ni heshima kuu sana kwake!

Brian amekuwa akishiriki katika Olimpiki Maalum za RI tangu awe katika shule ya upili. Pamoja na bocce anacheza michezo tofauti ikiwemo softiboli, mpira wa kandanda wa bendera, kandanda, voliboli, mpira wa kikapu, kroketi, na mchezo wa kuvingirisha mpira chini. Amepokea medali kadhaa za Dhahabu, Fedha na Shaba!

Mama wa Brian, Bi. Jane Johnson, ni Mfanyakazi wa Kijamii aliyestaafu ambaye kwa sasa ana hudumu kama Mwalimu Mbadala katika **Gilbert Stuart Middle School (GSMS)**. Mwaka 2021, Brian alikuja GSMS na kuongea na madarasa kadhaa kuhusu Olimpiki Maalum na umuhimu wa kujumuisha kwa watu wenye mahitaji maalum. Brian alielezea wanafunzi jinsi matumizi ya nene "R" ina kwaza wengine. Alipokelewa vyema na wanafunzi na kufanya marafiki kadhaa wakati wa matembezi.

Ndugu wa Brian, Bw. Dan Johnson, amekuwa Mwalimu wa Elimu Maalum katika Providence, kwa miaka 17. Dan anaunga mkono sana ndugu yake! Brian anaahidi kuwakilisha Rhode Island na Marekani kwa uwezo wake wote. Malengo yake ni kuleta Medali ya Dhahabu nyumbani na kutengeneza marafiki wapya!

SALAMU KWA NATHANAEL GREENE H.E.S.H.I.M.A. TIMU

Wanafunzi kutoka **timu ya Usawa na Uongozi ya Nathanael Greene** wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii katika miradi yao ya usawa. Nangoja kwa hamu kuwaona na timu za wanafunzi wote wa middle na shule ya upili katika Kongamano letu mnamo tarehe 2 Februari.

KUWASHEREHEKEA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo mazuri kila siku. Hapa kuna mifano michache.

WANAFUNZI WA HARRY KIZIRIAN STUDENTS WANATEMBELEA FRIARTOWN

Wanafunzi kutoka **Harry Kizirian Elementary** walipata nafasi kwenda kwa **Providence College** mpira wa kikapu cha wanawake wiki iliyopita. Walikuwa wanafurahia sana kuwa chuoni, kutazama shule, na kwa ukweli walikuwa na muda mzuri mchezoni! Wanafunzi wengine hata waliongea kuhusu kutaka kwenda hapo kwa chuo. Shukrani maalum kwa wafanyakazi katika Harry Kizirian kwa kufanya tukio hili kuwezekana kwa wanafunzi na PC Friars kwa kuwa nao kwa chuo.

WABUNIFU WA MCHEZO WANANG'ARA KATIKA E-CUBED

Wanafunzi wa **E-Cubed Academy** walishiriki katika mashindano ya ubunifu pamoja na wenzao katika mpango wa PTECH baada ya tukio la hivi majuzi shuleni. Wanafunzi wa teknolojia wanachagua michezo nne bora zaidi na kuzionyesha kwa walimu, wanafunzi na wageni. Watu wazima halafu wanaambiwa kujaribu michezo na kupigia kura wanaye mpenda zaidi. Hongera kwa wana kodi nne na hongera kuu kwa Jeffery Juarez, mwanafunzi wa darasa la tisa, ambaye alishinda mashindano ambapo mchezo wake ulio angazia grafiki za kidijitali za kuchorwa kwa mkono! Tazama mchezo wake hapa : http://ow.ly/bFI550Mv6Bv



KAZI YA KIKUNDI YA KUJUMUISHA

Wiki hii, wanafunzi wa Lugha Mbili wa darasa la nne katika **Lima Elementary**walijiunga kwa vikundi vya kujumuisha kuelezea moja ya sifa ya shule yao ya P.R.I.D.E P.R.I.D.E. inamaanisha Kuvumilia, Kuwajibika, Uadilifu, Madhubuti, na huruma. Kazi nzuri kwa Lima Lions kwa kufanya kazi pamoja na kuleta njia bunifu kujumuisha msemo wa shule yao!

MABINGWA WA CHESI

Hongera kwa wanafunzi wote wa PPSD ambao walishiriki katika Mashindano ya Shule ya Bure ya Chesi ya tatu ya **Classical High School** wiki uliopita! Wanafunzi Wilayani kote walikuja kushiriki. Hongera maalum kwa wanafunzi wafuatao ambao walikuwa kwa mashindano:

- Henry Eberman, nafasi ya kwanza, Classical
- Benjamin Giller, nafasi ya pili, Classical
- Jermaine Alston, nafasi ya tatu kuwa usawa, PCTA
- Pascal Kim, nafasi ya tatu usawa, Classical



KUANGAZIA WAFANYAKAZI

Pata kujua watu wazuri ajabu wanaofanya kazi na wanafunzi wetu kila siku!

Catherine M. Anderson (aka Mx. A)

Mwalimu wa darasa la 9 wa ELA na Ukuzaji wa Kuandika, Kiongozi wa Mwalimu wa Freshman, Mwana bodi wa Usawa wa Shule za Umma za Providence, Mshirika wa Fundisha kwa Kikundi cha Black Lives

Aliyeko: Hope High School

Alijiunga na PPSD mwaka: 2019

Ni nini kilicho kufanya ufanye kazi kama mwalimu wa ELA?

Katika darasa la kwanza, nilikuwa na mwalimu ambaye alichagua hadithi ambayo niliandika kutoka kwa maono ya turkey kuhusu kuogopa sherehe ya Shukrani kushiriki na darasa. Sifa zake, na furaha aliyo elezea katika msokoto wa hadithi na uchaguzi wa maneno ulikuwa inaeleweka. Katika shule ya kati, mwalimu wangu wa ELA wa darasa la nane aliniuliza ikiwa nitajiunga na klabu ya shairi alikuwa akitoa maonyesho, wakati nilipokuwa natengwa kijamii na nilikuwa na msongo. Bado niko na mkusanyiko wa kwanza (na wa mwisho) "iliyochapishwa", kikundi kisicho unganishwa cha maneno wasomi na yeye walifurahia sana katika kujenga pamoja. Halafu shule ya upili, wakati wa muda mgumu kwa familia yangu, mwalimu wangu wa ubinadamu alikuja kwa nyumba yangu kukumbusha wazazi wangu kwamba nguvu zangu zitang'ara katika mseto wa chuo, na kuwa mbali nao ndio ninalo hitaji. Nilikuwa kwa orodha ya mkuu wa cho katika muhula wa kwanza kwa chuo. Matukio haya yanakuza kwangu imani na mwalimu mwenye ufahamu na anayejali ambaye anaeza kuona na kusikia unaweza badilisha njia ya mtu njiani, (kwa hakika naamini pia kinyume ni ukweli kwa wengi ambao walikuwa na uzoefu kinyume na wangu, na ambao wamepoteza imani yao katika sauti yao wenyewe). Ulezi wangu wa upendeleo huko Washington, DC/ Virginia Kaskazini ilinipatia uzoefu mwingi mzuri, kama vile maonyesho ya ukumbi, makumbusho, maktaba ya umma, na kuzungukwa na marafiki wengi duniani kote ambao wali thamini sana uwezo wao wakujieleza, zote zilichangia katika upendo wangu wa lugha, elimu, na umuhimu wa kujifunza kutoka kwa watu wenye uzoefu tofauti na wangu wa maisha.

"Wanafunzi wanahitaji kuhisi salama, kushangiliwa na kuonekana wakati wanapo ingia kwa chumba."

Je, unaweza kuelezea vipi kazi yako kwa watu ambao hawafanyi kazi katika elimu?

Siwezi kuwa na heshima zaidi kwa wenzangu ambao walifundisha wakati wa janga (na ambao walibaki na walio chagua kutobaki) ambayo ilisababisha ubunifu wa kuendelea, huruma na uvumilivu. Katika siku yeyote leo, kuwa mwalimu inamaanisha kushughulikia kwa kuendelea katika athari kwa miaka mitatu iliyopita kwa wanafunzi, familia zao na jamii. Kutoka kwa mwonekano wa kielimu tunahitaji kutengeneza angalau marudio matatu kwa kila somo; moja kwa wanafunzi ambao wanaweza kuhudhuria shule kawaida (kama vile wanaweza kufikia usafiri unao aminika, hawatarajiwi kupeleka ndugu shuleni, au kwenda kazini kusaidia familia, n.k), moja kwa wanafunzi ambao watakuja kwa masomo machache ya mwisho kwa sababu zote zilizo orodheshwa hapo juu na sababu zingine, na nyingine kwa mwanafunzi ambaye anaweza kufikia kipimo cha kufika shuleni wiki chache tu, lakini bado ana hudhuria. Kila kategoria inahitaji mapendekezo kwa elimu maalum iliyotambuliwa na masomo ya lugha nyingi (kama vile kazi za shule ambazo ziko na usaidizi wa ziada ulio pachikwa kama vile toleo tofauti la ujumbe lenye msamiati, au uboreshaji wa mwonekano, au ishara za kurudiwa za usemi). Haya ni matofali ya ujenzi tu ya somo lolote linalo stahili. Halafu tunahitaji kuzingatia ni ujumbe gani wa ziada tunaweza na pia tuta jumuisha ambayo inafikia viwango sawia zilizo angaziwa lakini zinapeana wanafunzi na nyenzo zinazo zingatia utamaduni. Kwa mfano, katika kitengo cha majuzi sana kilicho angaziwa katika shairi la Mary Oliver na Robert Frost kutoka kwa mtaala, mimi na mwenzangu tulifundisha shairi la ziada la malenga wa Kuba kwa lugha ya Kihispania na Kiingereza ambayo iliashiria mada sawia na vipengele vya ziada vya ushairi. Tulisikiza na kusoma shairi kwa lugha ya Kihispania na Kiingereza.

Je, ungependa watu wengi kujua nini kuhusu kuwa mwalimu wa ELA?

Kuwa mwalimu wa ELA ni kuhusu kutengeneza mazingira ambapo wanafunzi wote wanahisi kwamba hadithi zao, mandhari nyuma yao, matarajio yao na changamoto zinalenga kwao na kutambuliwa ipasavyo. Wanafunzi wanahitaji kuhisi salama, kushangiliwa na kuonekana wakati wanapo ingia kwa chumba. Kuwa mwalimu wa ELA ni pia kifaa cha kuweka maji baridi, mimea, kochi ya sehemu yenye vitabu vya meza ya kahawa inayo onyesha wasanii wa rangi, nukuu za wanafunzi wengine kuhusu mafanikio ya wengine kwenye bodi na makubaliano yetu ya jumuiya. Kuwa mwalimu wa lugha ya Kiingereza ni kuwa na uangalifu wa faragha ukumbini wa mara kwa mara baada ya mtoto kushiriki kuhusu shambulizi la mhangaiko, kuvunjwa moyo au mwanafamilia mgonjwa. Siku zingine ni kufahamu wakati wa kuchukua mapumziko na kufanya utani wa baba au kutembea kiasi uwanjani. Mwanzo wa mwaka, ina maanisha kuonyesha udhaifu wango kwanza-kutaja makosa yangu na kushiriki mapendeleo yangu kuitwa "Bix" dhidi ya "Bi" kwa sababu, kama hao, nina mchanganyiko wa utambulisho. Ni mambo haya yote kuwa MWALIMU katika siku yeyote. Tofauti pekee na kile mwenzangu anafanya chini ya ukumbi na kikokotoo, kikombe, pensili ya makaa, metronome, ramani au jamvi la chumba cha mazoezi na kwamba lengo langu la mwisho ni kufanya wanafunzi wangu waweze kutaja njia walivyo endelea kama wasomi na waandishi. Wakati wanavyo kuwa na upekuzi zaidi kuhusu hao ni nani, na wewe ni nani ukiwa njiani.

Ni mambo gani yaliyoangaziwa mwaka huu kufikia sasa?

Kila siku niko darasani na kuona mwanafunzi ana tabasamu bila kizuizi ni jambo la kuangazia. Kufundisha na kusoma wakati wa janga ulipunguza na kuathiri kila mtu kwa njia zao wenyewe-zingine bado hatuja anza kupakua. Kwa hivyo kwangu, kuweza kuona uso wa mwanafunzi umeng'ara wakati wa "mshangao" kwa masomo yao, au hadithi ambayo rafiki ameshiriki, au muda ambao mwenzake amemaliza tu kusoma shairi mbele ya darasa ni miujiza kila wakati. Hatujawahi kuona sura za wenzetu ana kwa ana kwa kadiria miaka miwili. Hivi majuzi, kutazama michezo ya mpira wa kikapu, mechi za mieleka, na uzoefu wa mafanikio ya timu ya voliboli ya wasichana wetu imekuwa furaha kuu. Idara yetu bora ya Kiingereza imeongezewa walimu wanne hodari na wenye huruma na wagombeaji wanne hodari wa shahada ya uzamili ya Elimu ya Chuo kikuu cha Brown ambao wanatupatia motisha na kutuhamasisha kila siku. Kujifunza ukuaji mkuu na ufanisi katika ELA katika mwaka uliopita ilikuwa moja wapo ya sababu shule yetu ili tambuliwa hivi majuzi na pia alama nyingine ya juu kwa kila mtu.

Unatarajia nini kwa hamu kwa mwaka wote uliobaki?

Mimi ni mtu ambaye anajaribu kubaki ndani leo (kufundisha inahitaji mtindo huu kwa maoni yangu). Lakini kwa uhakika nangoja kwa hamu kuhitimu kwa Hope (kama wanafunzi wengi katika madarasa yangu ya kwanza katika Hope 2019 watakuwa wana vuka hatua hii), na ile ya mtoto wangu mwenyewe The Met. Hii ni wakati mzuri na mkali kwa ukweli kama sote tunavyo fahamu wakati wanafunzi wetu na watoto wetu wanaendelea na hatuhisi tena kuwa na uweza sawia kuwashauri au kuwahamasisha wakati wanapo paa. Pia ni furaha mno kushuhudia wakichukua hatua kwa dunia kuu kwa njia ambazo wao, au wewe, hungeweza kudhania miaka nne iliyopita. Nitakamilisha mpango wa kuhitimu kwa cheti cha MLL katika Chuo Kikuu cha Roger Williams kadiria wakati sawia. Nangoja kwa hamu kusaidia wanafunzi wangu kupanga kwa Saluni ya Umma ya Majira ya Chipuko (maonyesho ya modeli kadhaa na kusherekea kazi ambayo wana jivunia kimahususi au kutoka kwa mwaka) na kwa ukweli kupiga shangwe katika michezo ya majira ya chipuko (wanaipenda, hata kama wanajidai hawapendi!) Lakini mara nyingi, nangoja kwa hamu kuonekana kesho na kuona tabasamu nyingine, au kutazama mwanafunzi mwingine akishiriki nguvu zake maradufu na wenzake wakati wanapo jadiliana kuhusu jambo fulani.

NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI

- Shanell Smith-Akpan ni Mchezaji Bora wa Mpira wa Kikapu wa Wasichana wa Jarida cha Providence
  Jarida la Providence, Januari 13
- E-Cubed Academy, Providence High School Ina pokea Tuzo la Kitaifa Kutoka Code.Org
  Redio ya Coalition, Januari 12
- Mwalimu wa maeneo anashiriki uzoefu wake katika Jitihada ya URI
  WPRI, Disemba 8

WILAYANI

MASHUJAA WA MAHUDHURIO WA PPSD

Beth O'Day-Hall ni Mtaalamu Mkuu wa Jamii katika **Akademia ya Taaluma na Ufundi ya Providence**.
Ana tengeneza uhusiano na wanafunzi na familia zao kuhakikisha wanafunzi wanakuja shuleni kila siku. Bofya kwenye video hapa kujifunza zaidi kuhusu huyu Shujaa wa Mahudhurio, na jinsi unavyo weza kushiriki!

E-CUBED INASHINDA RUZUKU YA SAYANSI YA KOMPYUTA YA $10K

Hongera kwa **E-Cubed Academy** kwa kushinda ruzuku ya $ 10, 000 kwa masomo ya sayansi ya kompyuta! E-Cubed ilikuwa ndio shule pekee katika Providence kupokea ruzuku hiyo, na pia shule moja kati ya tatu katika jimbo lote kupokea ruzuku. Shukrani maalum kwa Code.org kwa kutambua E-Cubed kwa tuzo hili la thamani, na mwalimu Ivelisse Sabater wa E-Cubed Lugha ya Dunia kushinda tuzo hili. Unaweza kusoma zaidi kuhusu tuzo hili katika tovuti ya PPSD.

SHULE INA SHEREKEA SIKU YA 80 SHULENI

Shule Wilayani kote walionyesha kiburi chao cha '80' hivi majuzi kusaidia kusherekea mwaka wa shule wa siku 80 shuleni. Wanafunzi na wafanyakazi walijiingiza katika hali ya kuvaa mavazi na mitindo ya nywele ya kushangaza. Wafanyakazi katika **Fogarty Elementary School** ni mfano tu wa mavazi yenye rangi yaliyo onekana. Tazama mwalimu wa sanaa Bw. Lundgren!

VIDOKEZO VYA USALAMA VYA MWANAFUNZI

Usalama wa mwanafunzi kwa kawaida ni kipau mbele katika Shule za Umma za Providence. Familia wanahimizwa kusoma ukumbusho wa usalama hapa chini kutoka kwa timu ya Usalama wa Chuo na kujadili pamoja na wanafunzi. Vidokezo hivi vya usalama zinalenga hususan wanafunzi ambao wanatembea, lakini wanaangalia vidokezo vya ziada vya usalama katika sehemu hii ya kijarida mara kwa mara siku za baadaye.
Wanafunzi huhisi vyema katika sehemu ambazo wana tembelea mara kwa mara na huwa hawako makini kwa mazingira yao kila muda. Ukiwa na hiyo mawazoni, hizi ni baadhi ya alama za kuongea kujadili na mwanafunzi wako ikiwa wanatembea kwenda shuleni.

- ✓ **NJIA SALAMA**
  - ⇨ Chagua njia ya shule yenye mwangaza bora na sehemu yenye shughuli nyingi
  - ⇨ Tembea njia hii na mtoto/watoto wako ili nyote kufahamu njia hiyo kwenda na kutoka shuleni.
- ✓ **KUTEMBEA NA MARAFIKI**
  - ⇨ Jaribu kutembea kwa kikundi kuliko kutembea peke yako
  - ⇨ Hakikisha marafiki wanakusanyika pamoja na sio kando wakati wa kwenda na kurudi kutoka shule.
- ✓ **SEHEMU SALAMA**
  - ⇨ Onyesha maduka na nyumba zinazo julikana ambapo marafiki/familia wanapoishi ambazo ziko njiani au karibu.
- ✓ **TEKNOLOJIA**
  - ⇨ Epuka kuwa na simu kwa maonyesho, kwa vile hii inaweza changanyisha mtu na kuwezekana kuwa hatari ya kulengwa kwa uwizi.
  - ⇨ Epuka kutumia visikizi/vifaa vya kusikiliza, kwa vile inaweza kukuzubaisha kutoka kwa mazingira yako na pia kuwezekana kuwa hatari ya kulengwa ya uwizi
- ✓ **SHERIA YA "MWEREVU HAENDI KAMWE"**
  - ⇨ Watoto hawapaswi kwenda popote na MTU YEYOTE-hata kama wana wajua-ikiwa haijakubaliwa kwa mapema kupitia mzazi au mlezi.
  - ⇨ Epuka kwa upole kuuliza mtu yeyote kwa msaada ambayo ina watoa sehemu ambapo wanaishi kwa sasa. Mifano inaweza kuwa kuitisha usaidizi wa kutafuta mbwa aliyepotea, usaidizi unao hitajika kusongesha kitu au wazazi wako walisema ni sawa mimi kukubeba.
- ✓ **TUMIA SAUTI YAKO**
  - ⇨ Katika kujilinda mwenyewe matumizi ya sauti yako inaweza kuwa kifaa chenye nguvu sana. Ikiwa mtoto wako hahisi salama wakati mtu anapo mkaribia, wanapaswa kupaza sauti kufahamisha watu na pia kuepusha mtu huyu kumpatia wasi wasi.
- ✓ **TENGENEZA VIDOKEZO**
  - ⇨ Ikiwa mto yeyote anashuhudia au kuona jambo ambalo haliko sawa, tengeneza vidokezo na kuandika taarifa nyingi iwezekanavyo na kuripoti kwa wazazi/walimu. Tengeneza vidokezo vya mtu husika, maeneo, muda , gari walimo ingia, andika taarifa nyingi iwezekanavyo.

WEKA ALAMA KWA KALENDA YAKO!

- **SIKU YA KUONDOKA MAPEMA**
  Jumatano, tarehe 25 Januari
- **MAONYESHO YA KANDARASI YA AJIRI YA MAPEMA**
  Alhamisi, tarehe 26 Januari
  9:00 a.m. hadi 11:00 a.m.
  Jengo la Usimamizi

Mambo ya kusisimua yanatokea katika Wilaya nzima, na tunataka kueneza ujumbe! ikiwa una programu, hafla, mfanyakazi, au mwanafunzi mwenye hadithi nzuri ajabu ambayo ungependa kuonyesha, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.

Providence Schools

© 2022 Providence Public Schools · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org